

Heureux ceux qui procurent la paix

Par Gary E. Stevenson
du Collège des douze apôtres

Heri Wapatanishi

Na Mzee Gary E. Stevenson
Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

Conférence générale d'octobre 2025

Pour être un artisan de paix, tout commence à l'essentiel, dans notre cœur. Ensuite, dans notre foyer et notre famille.

Bienvenue à la conférence générale. Combien nous sommes reconnaissants d'être ensemble.

Alors que nous entamons cette conférence, nous gardons à l'esprit les événements douloureux des semaines qui l'ont précédée. Nos cœurs sont lourds à cause du deuil ou, pour certains, de l'incertitude persistante causée par la violence et les tragédies dans le monde. Même des personnes pieuses rassemblées dans des lieux sacrés, y compris notre église consacrée au Michigan, ont perdu la vie ou des êtres chers. Je vous parle avec mon cœur, conscient des fardeaux que votre famille et vous portez et de ce que notre monde a subi depuis la dernière conférence générale.

Capernaüm en Galilée

Imaginez que vous êtes un adolescent à Capernaüm, près de la mer de Galilée, pendant le ministère de Jésus-Christ. Des rumeurs se répandent au sujet d'un rabbi, ou instructeur, dont le message attire les foules. Des voisins prévoient de se rendre sur une colline surplombant la mer pour l'écouter.

Vous parcourez avec eux les routes poussiéreuses de Galilée. En arrivant, vous êtes étonné par la taille de la foule rassemblée pour écouter ce Jésus. Certains murmurent le mot « Messie ».

Vous écoutez. Ses paroles touchent votre cœur. Sur le long chemin de retour chez vous, vous préférez le silence aux conversations.

Upatanishi bado unaanzia mahala pa muhimu zaidi—ndani ya mioyo yetu. Kisha nyumbani na kwenye familia.

Karibuni kwenye mkutano mkuu. Tunashukuru jinsi gani kwa kukusanyika.

Tunapotazamia matangazo haya ya mkutano, tunafahamu vyema juu ya wiki zilizotangulia hili. Tunatambua kwamba mioyo mingi inaomboleza kwa upotevu, na baadhi wanahisi kutokuwa na uhakika kunakosababishwa na vurugu au majanga kote ulimwenguni. Hata watu wacha Mungu waliokusanyika katika sehemu takatifu—ikijumuisha kanisa takatifu katika Michigan—wamepoteza maisha yao au wapendwa wao. Ninazungumza kutoka ndani ya moyo wangu, nikitambua kwamba mingi ya mioyo yenu imelemewa na kile ambacho ninyi, familia zenu, au ulimwengu wetu umepitia tangu mkutano mkuu uliopita.

Kapernaumu Galilaya

Vuta taswira pamoja nami kwamba wewe ni kijana katika Kapernaumu, kando ya Bahari ya Galilaya, wakati wa huduma ya Yesu Kristo. Taarifa zinasambaa kuhusu rabi—mwalimu—ambaye ujumbe wake unawavuta wengi. Majirani wanapanga kusafiri kwenda mlima ulio mkabala na bahari ili kumsikiliza.

Unaungana na wengine kutembea katika njia yenye vumbi ya Galilaya. Unapofika, umati mkubwa uliokusanyika kumsikiliza huyu Yesu unakushangaza. Baadhi wananong'ona kwa upole, "Masiya."

Unasikiliza. Maneno Yake yanaugusa moyo wako. Kwenye matembezi marefu ya kurudi nyumbani, unachagua ukimya badala ya mazu-

Vous méditez sur des choses merveilleuses, qui transcendent la loi de Moïse elle-même. Il a parlé de tendre l'autre joue et d'aimer ses ennemis. Il a promis : « Heureux ceux qui procurent la paix, car ils seront appelés enfants de Dieu. »

Pourtant, sous le poids des jours difficiles, de l'incertitude et de la peur, la paix semble bien loin.

Vous accélérez le pas et arrivez chez vous le souffle court. Votre famille se rassemble et votre père vous demande ce que vous avez entendu et ressenti.

Vous rapportez qu'il vous a invités à laisser votre lumière luire devant autrui, à rester droit malgré les persécutions. Votre émotion est audible quand vous répétez : « Heureux ceux qui procurent la paix, car ils seront appelés enfants de Dieu. »

Vous demandez : « Puis-je réellement devenir un artisan de paix dans un monde en tumulte, alors que la peur habite mon cœur et que la paix semble si lointaine ? »

Votre père regarde votre mère et répond avec douceur : « Oui. Tout commence à l'endroit le plus essentiel : notre cœur. Ensuite, notre foyer et notre famille. Et ce que nous mettons en pratique ici se répand alors dans nos rues et nos villages. »

2 000 ans plus tard

Avançons de 2 000 ans. Il ne s'agit plus d'un exercice d'imagination, mais de notre réalité. Certes, les pressions ressenties par la génération montante (la polarisation, la sécularisation, les représailles, la violence au volant, les scandales, les attaques groupées sur les réseaux sociaux) diffèrent de celles du jeune de Galilée. Néanmoins, les deux générations sont confrontées à des cultures marquées par le conflit et les tensions.

Heureusement, nos jeunes gens et jeunes filles sont aussi attirés par des sermons sur la montagne modernes : le séminaire, les conférences Jeunes, Soyez forts et Viens et suis-moi. Ils reçoivent les mêmes invitations du Seigneur : laisser leur lumière luire devant autrui, rester droits malgré les persécutionset aimer leurs ennemis.

Les prophètes actuels du Rétablissement les ont encouragés à être des artisans de paix, à exprimer leur désaccord sans être désagréables,

ngumzo.

Unatafakari mambo ya kustaajabisha—mambo ambayo ni zaidi hata ya sheria ya Musa. Alizungumza kuhusu kugeuza shavu lingine na kuwapenda maadui zako. Aliahidi, “Heri wapatanishi: maana hao wataitwa wana wa Mungu.”

Katika uhalisia wako, kadiri unavyohisi uzito wa siku ngumu—kutokuwa na uhakika na hofu—amani inaonekana kutofikika.

Hatua zako zinaongezeka; unafika nyumba ni umechoka sana. Familia yako inakusanyika; baba yako anauliza, “Tuambie kile ulichosikia na kuhisi.”

Unashiriki kwamba Alikualika kuacha nuru yako iangaze mbele za watu, kutafuta haki hata wakati unapoudhiwa. Sauti yako inatetemeka unaporudia, “Heri wapatanishi: maana hao wataitwa wana wa Mungu.”

Unauliza, “Ninaweza kweli kuwa mpatanishi wakati ulimwengu upo katika vurugu, wakati moyo wangu umejaa hofu, na wakati amani inaonekana kutofikika?”

Baba yako anamtazama mama yako na kujibu kwa upole, “Ndiyo. Tunaanzia mahali pa muhimu zaidi—ndani ya mioyo yetu. Kisha kwenye nyumba na familia zetu. Tunapofanya mazoezi huko, upatanishi unaweza kusambaa kwenye mitaa na vijiji vyetu.

Peleka Mbele Miaka 2,000

Peleka mbele miaka 2,000. Hakuna haja ya kuvuta taswira—huu ni uhalisia wetu. Ingawa mashinikizo yanayohisiwa na kizazi chipukizi cha leo ni tofauti na yale ya kijana katika Galilaya—ubaguzi, ukosefu wa dini, visasi, hasira barabarani, jeuri, na mashambulizi kwenye mitandao ya kijamii—vizazi vyote viwili vinakabiliana na tamaduni za migogoro na mashinikizo.

Kwa shukrani, wavulana na wasichana wetu kadhalika wameletwa kwenye nyakati zao za Mahubiri ya Mlimani: seminari, mikutano ya Kwa Ajili ya Nguvu kwa Vijana, na Njoo, Unifuute. Hapa wanapokea mialiko sawa ya kudumu kutoka kwa Bwana: kuacha nuru yao iangaze mbele za watu, kutafuta haki hata wakati wanapoudhiwa, na kuwapenda maadui zao.

Wanapokea pia maneno ya kutia moyo kutoka kwa manabii walio hai wa Urejesho: “Wapatanishi Wanahitajika.” Kuwa na maoni tofauti bila

à remplacer les querelles et l'orgueil par le pardon et l'amour et à construire des ponts de compréhension et de coopération plutôt que des murs de préjugés et de ségrégation. Et ils ont la même promesse : « Heureux ceux qui procurent la paix, car ils seront appelés enfants de Dieu. »

Le cœur de la génération montante actuelle est rempli du témoignage de Jésus-Christ et d'espérance pour l'avenir. Toutefois, ils demandent aussi : « Puis-je réellement devenir un artisan de paix dans un monde en tumulte, alors que la peur habite mon cœur et que la paix semble si lointaine ? »

La réponse est encore un oui retentissant ! Nous nous saisissons des paroles du Sauveur : « Je vous laisse la paix, je vous donne ma paix. [...] Que votre cœur ne se trouble point, et ne s'alarme point. »

Pour être un artisan de paix, tout commence à l'essentiel, dans notre cœur. Ensuite, dans notre foyer et notre famille. Ce que nous mettons en pratique là se répand ensuite dans le voisinage et les collectivités.

Voyons ces trois endroits où un saint des derniers jours de notre époque peut apporter la paix.

Être un artisan de paix dans son cœur

Le premier est notre cœur. Il est clair que les enfants étaient attirés par le Christ pendant son ministère. Il y a là un indice. Le cœur pur et innocent d'un enfant qui procure la paix est une source d'inspiration pour notre cœur. Voici la réponse de plusieurs enfants en âge d'aller à la Primaire à la question : « Comment être un artisan de paix ? »

Leurs réponses venaient du cœur. Luke a dit : « Il faut toujours aider les gens. » Grace a expliqué qu'il est important de pardonner, même lorsque cela ne semble pas juste. Anna a raconté : « J'ai vu une fille qui jouait toute seule, alors je suis allée jouer avec elle. » Lindy pense qu'être un artisan de paix signifie aider quelqu'un. « Et la personne aide à son tour. Et ça continue à l'infini. » Liam a dit : « Il ne faut pas être méchant avec quelqu'un qui est méchant avec nous. » London s'est exclamée : « Si quelqu'un se moque de toi ou est méchant, dis-lui : 'Arrête, s'il te plaît.' » Trevor a expliqué : « S'il ne reste qu'un beignet et que tout le monde le veut, on le partage. »

Les réponses de ces enfants me prouvent que

kuwa adui. Badilisha ubishi na kiburi kwa msa-maha na upendo. Jenga madaraja ya ushirikiano na uelewa, si kuta za chuki au ubaguzi. Na ahadi ileile: “Heri wapatanishi: maana hao wataitwa wana wa Mungu.”

Mioyo ya kizazi chipukizi cha leo imejaa ushuhuda wa Yesu Kristo na tumaini kwa ajili ya siku zijazo. Na bado wao pia wanauliza, “Ni-naweza kweli kuwa mpatanishi wakati ulimwen-gu upo katika vurugu, moyo wangu umejaa hofu, na amani inaonekana kutofikika?”

Jibu imara kwa mara nyingine ni ndiyo! Tunayakubali maneno ya Mwokozi: “Amani nawaachieni; amani yangu nawapa. ... Msifad-haike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga.”

Upatanishi bado unaanzia mahala pa muhimu zaidi—ndani ya mioyo yetu. Kisha nyumbani na kwenye familia. Tunapofanya ma-zoezi huko, upatanishi utasambaa katika ujirani na jumuiya zetu.

Hebu tuzingatia zaidi maeneo haya matatu ambapo Mtakatifu wa Siku za Mwisho wa leo “anakuwa mpatanishi .

Upatanishi Ndani ya Mioyo Yetu

Kwanza ni ndani ya mioyo yetu. Kipengele cha wazi cha huduma ya Kristo kinaelezea jinsi watoto walivyovutiwa Naye. Hapo ndipo ki-dokezo kilipo. Kutazama ndani ya moyo msafi na usio na hatia wa upatanishi wa mtoto inaweza kuwa uvuvio kwa mioyo yetu. Hivi ndivyo watoto kadhaa wa umri wa Msingi walivyojibu “Inaonekanaje kuwa mpatanishi?”

Ninashiriki majibu yao moja kwa moja kutoka mioyoni mwao! Luke alisema, “Daima wasaidie wengine.” Grace alishiriki jinsi ilivyo muhimu kusameheana, hata wakati ambapo haonekani kuwa sawa. Anna alisema, “Nilim-wona mtu ambaye hana wa kucheza naye, hivyo nilienda kucheza naye.” Lindy alisema kwamba kuwa mpatanishi ni kuwasaidia wengine. “Ki-sha unasongesha hilo mbele. Litaendelea mbele tena na tena.” Liam alisema, “Usiwe mkorofi kwa watu, hata kama wao ni wakorofi kwako.” Lon-don alisema kwa msisitizo, “Ikiwa mtu anafanya mzaha au ni mkorofi, unasema, ‘Tafadhali acha.’” Trevor alisema, “Ikiwa kuna donati moja imebaki na wote mnaitaka, mnagawana.”

Majibu ya watoto hawa ni ushahidi kwan-

nous naissons tous avec un attrait divin pour la gentillesse et la compassion. L'Évangile de Jésus-Christ nourrit ces caractéristiques divines, notamment celle d'être un artisan de paix, et les ancre dans notre cœur, pour notre profit dans cette vie et dans la suivante.

Être un artisan de paix chez soi

Deuxièmement, nous sommes des artisans de paix chez nous lorsque nous nous conformons au modèle du Seigneur dans nos relations : la persuasion, la longanimité, la gentillesse, la douceur et l'amour sincère.

Voici l'histoire inspirante d'une famille dont les membres se sont efforcés d'être des artisans de paix et de mettre ces principes en action.

Les enfants de cette famille avaient du mal à tisser des liens avec un adulte souvent grincheux, condescendant et brusque. Les enfants, blessés et frustrés, se sont demandé si la seule solution était d'imiter cette attitude mesquine.

Un soir, la famille a discuté ouvertement de ces tensions et des dégâts qu'elles causaient. Une idée s'est présentée : pas une simple solution, mais une expérience à faire.

Au lieu de s'abstenir de répondre ou de contre-attaquer, les enfants feraient quelque chose d'inattendu : ils répondraient avec gentillesse. Pas seulement une retenue polie, mais un déversement délibéré de mots doux et d'attentions, peu importe la réaction. Ils ont tous accepté d'essayer pendant un moment, puis de se réunir à nouveau pour en reparler.

Malgré une légère hésitation au départ, ils se sont attachés à ce plan de bon cœur.

Le résultat a été tout simplement remarquable.

La froideur a commencé à fondre. Les sourires ont remplacé les airs renfrognés. L'adulte, autrefois distant et sévère, a commencé à changer. Les enfants, encouragés par leur choix de montrer l'exemple avec amour, se sont réjouis de la transformation. Le changement a été si profond que le moment de se réunir pour en reparler n'est jamais venu. La gentillesse avait fait son œuvre en douceur.

Des liens d'amitié sincère se sont formés et tout le monde a été édifié. En tant qu'artisans de paix, nous pardonnons et nous cherchons à édifier les gens plutôt qu'à les rabaisser.

gu kwamba sote tumezaliwa na tabia ya asili ya kiungu ya ukarimu na huruma. Injili ya Yesu Kristo hukuza na kufuma pamoja tabia hizi za kiungu, ikijumuisha upatanishi, ndani ya mioyo yetu, zikitubariki katika maisha haya na yajayo.

Upatanishi Nyumbani

Pili, kujenga upatanishi ndani ya nyumba zetu kwa kutumia mpangilio wa Bwana kushawishi mahusiano kati yetu: ushawishi, uvumilivu, upole, ukarimu, unyenyekevu na upendo usio unafiki.

Hapa kuna hadithi ya kuvutia inayoelezea jinsi familia moja ilivyofanya upatanishi kuwa lengo la pamoja, wakifanyia kazi kanuni hizi.

Watoto katika familia hii walikuwa wakipata shida katika uhusiano wao na mtu ambaye tabia yake mara nyingi ilikuwa hasira, kujikweza, na ukali. Watoto, wakiumizwa na kukasirishwa, walianza kujiuliza ikiwa njia pekee ilikuwa ni kuiga tabia zilezile za roho ya ukatili.

Jioni familia ilizungumza kwa uwazi pamoja kuhusu hali ile na madhara yake. Na kisha wazo likaibuka—si tu suluhisho bali jaribio.

Badala ya kujibu kwa ukimya au kisasi, watoto wangepanya jambo lisilotarajiwa: wangepibu kwa ukarimu. Si tu kujizuia kwa upole bali utoaji wa makusudi, kutoka moyoni wa maneno ya ukarimu na matendo ya kujali, bila kujali malipo yake. Wote walikubali kujaribu kwa muda fulani, ambapo baadaye wangekutana tena na kujadili.

Ingawa baadhi mwanzoni walisita, walijikita kwenye mpango kwa moyo wa dhati.

Kilichotokea baadaye kilikuwa cha kustaajabisha.

Uadui ulianza kupungua. Tabasamu zikachukua nafasi ya hasira. Mtu mzima yule, aliyekuwa adui na mkali, alianza kubadilika. Watoto, wakipewa nguvu na uchaguzi wao wa kuongoza kwa upendo, walipata shangwe katika badiliko. Badiliko lilikuwa kubwa kiasi kwamba mkutano wa ufuatiliaji uliopangwa haukuhitajika. Ukarimu ulikuwa umefanya kazi yake ya kimya kimya.

Baada ya muda, miunganiko ya kweli ya urafiki ilijengwa, ikimuinua kila mmoja. Ili kuwa wapatanishi, tunawasamehe wengine na kwa makusudi kuwainua wengine badala ya kuwashusha chini.

Être un artisan de paix dans sa collectivité

Troisièmement, soyons des artisans de paix dans notre collectivité. Pendant les années difficiles de la Seconde Guerre mondiale, John A. Widtsoe a dit : « La seule manière de créer une communauté paisible, c'est de former des hommes et des femmes qui aiment et font régner la paix. Chaque personne, par cette doctrine du Christ, [...] a entre ses mains la paix du monde. »

La belle histoire suivante illustre ce précepte.

Il y a quelques années, un imam et un pasteur du Nigeria se trouvaient de part et d'autre d'un fossé religieux. Chaque partie avait grandement souffert. Pourtant, par le pouvoir guérisseur du pardon, ils ont choisi d'avancer ensemble.

L'imam Muhammad Ashafa et le pasteur James Wuye sont devenus des amis et des partenaires de la paix. Ils ont fondé un centre pour la médiation entre les religions. Ils incitent maintenant d'autres personnes à remplacer la haine par l'espérance. Deux fois nominés pour le prix Nobel de la paix, ils ont récemment reçu le premier prix de la paix du Commonwealth.

Ces anciens ennemis voyagent maintenant côte à côte, rebâtissant ce qui a été détruit. Ils sont des témoins vivants que l'invitation du Sauveur à être des artisans de paix est non seulement possible, mais aussi puissante.

Quand nous découvrons la gloire de Dieu, nous ne sommes « pas enclins à [nous] nuire les uns aux autres, mais à vivre en paix ». Dans nos assemblées et nos collectivités, choisissons de nous voir les uns les autres comme des enfants de Dieu.

Programme d'une semaine pour procurer la paix

Pour résumer, je vous lance une invitation. Pour être un artisan de paix, il faut agir. Qu'allons-nous faire, individuellement, dès demain ? Je vous propose un programme d'une semaine, en trois étapes, pour être des artisans de paix.

Un foyer sans querelles : Quand une dispute commence, arrêtez-vous et reprenez du début avec des mots doux et des attentions aimantes.

Construisez des ponts numériques : Avant une publication en ligne, une réponse ou un

Upatanishi kwenye Jumuiya Zetu

Tatu, upatanishi kwenye jumuiya zetu. Katika miaka ya dhiki ya Vita ya Pili ya Dunia, Mzee John A. Widtsoe alifundisha: “Njia pekee ya kujenga jumuiya yenye amani ni kuwajenga wanaume na wanawake wenye upendo na wapatanishi. Kila mmoja, kwa fundisho hilo la Kristo ... anashikilia mikononi mwake amani ya ulimwengu [mzima].”

Hadithi ifuatayo inaelezea kwa uzuri mstari huo.

Miaka kadhaa iliyopita, wanaume wawili—imamu wa Kiislamu na Pasta wa Kikristo kutoka Nigeria—walisimama pande mkabala za mgawanyo mchungu wa kidini. Kila mmoja alikuwa ameteseka sana. Na bado, kupitia nguvu ya uponyaji ya msamaha, walichagua kutembea pamoja.

Imamu Muhammad Ashafa na Pasta James Wuye walikuwa marafiki na washirika ambao hawakutarajiwa wa amani. Kwa pamoja walianzisha kituo kwa ajili ya upatanishi wa mchanganyiko wa dini. Sasa wanawafundisha wengine kubadilisha chuki kwa tumaini. Wakiwa wameteuliwa mara mbili kwa ajili ya Tuzo ya Amani ya Nobel, hivi karibuni wamekuwa wapokeaji wa uzinduzi wa Tuzo ya Amani ya Jumuiya ya Madola.

Maadui hawa wa zamani sasa wanasafiri bega kwa bega kujenga kile kilichovunjika, ushahidi hai kwamba mwaliko wa Mwokozi wa kuwa wapatanishi si tu unawezekana—bali pia una nguvu.

Tunapopata kuujua utukufu wa Mungu, ndipo, “hatutakuwa na nia ya kuumizana, bali kuishi kwa amani.” Katika mikusanyiko yetu na jumuiya, na tuchague kutazamana kama watoto wa Mungu.

Mpango wa Wiki Moja wa Mpatanishi

Kwa ufupi, ninatoa mwaliko. Upatanishi unahitaji tendo—tendo hilo laweza kuwa lipi, kwa kila mmoja wetu, kuanzia kesho? Je, unaweza kuzingatia mpango wa wiki moja, wenye hatua tatu wa mpatanishi?

Nyumba isiyo na mabishano: Wakati mabishano yanapoanza, tulia na anza upya kwa maneno na matendo ya ukarimu.

Kujenga maelewano mtandaoni: Kabla ya kuposti, kujibu, au kutoa maoni mtandaoni, uli-

commentaire, posez-vous la question : « Vais-je construire un pont ? » Sinon, arrêtez-vous. Ne l'envoyez pas. Répandez plutôt la bonté. Publiez la paix au lieu de la haine.

Réparez et réunissez : Chaque membre de la famille tend la main à une personne avec qui la relation s'est détériorée pour s'excuser, servir, réparer et réunir.

Conclusion

Cela fait plusieurs mois que je me sens indéniablement poussé à transmettre ce message : « Heureux ceux qui procurent la paix. » Pour finir, je voudrais faire part de quelques impressions qui me sont venues pendant cette période.

Être un artisan de paix est une vertu chrétienne. Les artisans de paix sont parfois qualifiés de naïfs ou de faibles par diverses personnes. Pourtant, être un artisan de paix n'est pas une faiblesse, mais une force que le monde ne comprend pas toujours. Être un artisan de paix demande du courage et nécessite des compromis, pas le sacrifice des principes. Un artisan de paix dirige avec le cœur ouvert et non l'esprit fermé. Il approche autrui avec les mains tendues, pas les poings serrés. Être un artisan de paix n'est pas une nouvelle mode. Ce principe a été enseigné par Jésus-Christ lui-même, dans la Bible et dans le Livre de Mormon. Il a depuis été enseigné par les prophètes modernes, depuis les premiers jours du Rétablissement jusqu'à aujourd'hui.

Nous remplissons notre rôle divin d'enfant d'un Père céleste aimant en nous efforçant d'être des artisans de paix. Je témoigne de Jésus-Christ, le Prince de la Paix, le Fils du Dieu vivant, au nom de Jésus-Christ. Amen.

za, Je hili litaleta maelewano? Ikiwa halileti, acha. Usitume. Badala yake, shiriki wema. Tangaza amani mahala pa chuki.

Rekebisha na unganisha tena: Kila mwanafamilia angeweza kutafuta uhusiano uliovunjika ili kuomba msamaha, kuhudumu, kurekebisha, na kuunganisha.

Hitimisho

Imekuwa miezi kadhaa tangu nilipohisi msukumo usioepukika ulioongoza kwenye ujumbe huu: "Heri Wapatanishi." Katika kuhitimisha, naomba nishiriki misukumo ambayo imekuja moyoni mwangu kwa kipindi hiki.

Upatanishi ni sifa kama ya Kristo. Wapatanishi nyakati zingine wanaitwa washamba au dhaifu—katika hali zote. Lakini bado, kuwa mpatanishi si kuwa dhaifu bali ni kuwa imara katika njia ambayo ulimwengu hauielewi. Upatanishi huitaji ujasiri na mwafaka lakini hauhitaji dhabihu ya kuvunja maadili. Upatanishi ni kuongoza kwa moyo mkunjufu, si kukataa mawazo mapya. Ni kufikiana kwa mikono iliyonyooshwa, si ngumi zilizokunjwa. Upatanishi si jambo jipya, la moto kutoka kwenye mashine. Lilifundishwa na Yesu Kristo Mwenyewe, kwa wale walio kwenye Biblia na Kitabu cha Mormon. Upatanishi tangu hapo umefundishwa na manabii wa siku za leo tangu siku za mwanzo za Urejesho hata hivi leo.

Tunatimiza jukumu letu la kiungu kama watoto wa Baba wa Mbinguni mwenye upendo kadiri tunavyojitahidi kuwa wapatanishi. Ninashuhudia juu ya Yesu Kristo, ambaye ni Mfalme wa Amani, Mwana wa Mungu aliye hai, katika jina la Yesu Kristo, amina.